INSHA: BARUA KUTOKA MTAANI

MWANDISHI: Elias Shelukindo| eliasbenjaminshelukindo@gmail.com

Fungueni pazia mtazame filamu ya ghazabu. Filamu ambayo wahusika wake ni watoto wa mtaani. Watazameni namna wanavyoepuka kifo. Hapana msizifunge mboni zenu, tazameni. Tazameni namna ambavyo wanahukumiwa. Mtoto wa mtaani hana wazazi, wala walezi. Vipi tunawahukumu kwa mawe na faru pale tukiwakamata katika uwizi?. Msinielewe vibaya, wizi sio tabia nje ila waungwana tujiulizeni. Tujiulizeni kama tabia nzuri tunazotaka tuzione kwao, tuliwahi kuwafundisha?. Hii ni barua fupi ambayo wameniomba niwaandikie. Walitamani kuandika wenyewe, lakini wala elimu haipo katika vichwa vyao.

Mtoto wa mtaani amezaliwa kama ambavyo sisi tumezaliwa, pia amezaliwa na mwanamke kama ilivyo kwa wengine. Tafrani hujitokeza katika malezi yao. Hii ndio sababu ya kila baya mnalolisema kutoka kwao. Mtoto wa mtaani anaweza akawa yule aliyetelekezwa na mzazi wake ama yule ambaye wazazi wake wamepoteza maisha katika namna tofauti na kumwacha peke yake katika hii dunia. Dunia isyojali. Mitaa nayo kwa ukarimu ikawapokea, ikawafundisha maisha ambayo huenda hayakuwa yao. Lakini wangetenda kipi ikiwa na sisi tulijitenga nao?. Mitaa ikawalea, wizi ukawapokea. Wachache kati yao wakanusurika katika dimbwi hili, wakaokolewa na mashirika ya kulea watoto yatima, ila wengine wakabakia. Hawa ndio wameniambia niandike hii barua. Hawa waliobakia.

Maisha yao katikati ya mitaa ni kitendawili ambacho kisipoteguliwa kwa wizi basi watalala njaa. Hawana kazi, hawana mashamba ambayo wangeenda kupanda maindi wavune. Aridhi yao halali ni majalala, huku wakimendea lolote lile katika vichochoro. Mahitaji muhimu kwao ni habari ya kusadikika tu, na wala haipo katika hii dunia. Miili yao

Edit with WPS Office

inasitiriwa matambara yaliyojichokea, nyao za miguu yao zinafahamu kila ladha ya maumivu, jua kwa vipande vya chupa. Ugumu huu wamaisha unawapeleka katika vituo vya magari, sokoni na popote kule wanapoamini wanaweza kusogeza siku. Nia yao haikuwa kwenda kuiba, bali kuomba. Kuomba kulivyokuwa kugumu, wangefanya nini sasa?. Wafe na njaa?. Hapana!, wakagoma ndipo hapo kila baada ya dakika chache katika masoko na vituo vya mabasi utasikia mayowee ya uwizi.

Mtoto wa mtaani anakufa kila leo, akiponyoka katika kifo wakati akijitafutia chakula basi maradhi yatakatisha uhai wake. Nani anajali?. Mwili wake unazikwa, maisha yanaendelea. Mithili ya kisu kikali, maisha yao yanawakata, wapo ambao wameyakatisha maisha yao kwa kujinyonga. Wameamua kuikimbia dunia isiyowatambua kama sehemu yao. Wamechoka manyanyaso, kila kona matusi ni yao, watu wanaojiita wenye hadhi wakiwatukana watoke mbele yao, eti wanatia kinyaa. Waungwana wameniomba niandike mengi sana. Wamesema nisione aibu kusema kila walichoniambia. Wanataka hii barua iwafikie wengi, wengi ambao wameanza kuamini kuwa wao ni wahalifu.

Mtoto wa kike wa mtaani, yeye angekikwepa kifo wakati wa kujitafutia chakula jaani kwa kuikwepa misumari na chupa zilizovunjika. Ila mwishoye anakumbana na kirusi cha ukimwi. Ukimwi ambao wanaupata kwa kubakwa katikati ya kiza katika vichochoro ambavyo ndipo yalipo makazi yao. “mtoto anazaa mtoto” hii kauli inakamilishwa na matokeo ya kubakwa kwa mtoto wa kike wa mtaani. Miezi tisa inapokamilika kuna mawili, kupona ama kufa wakati wa kujifungua. Wengi wao wamekufa kwa kukosa huduma sahihi za uzazi wakati wa kujifungua, kwanza hizo huduma za afya wangezipata vipi katika vichochoro?. Yote haya wala hatutaki kuyaona, tunachokiona ni tabia mbaya kwao.

Ndugu zangu, mtoto wa mtaani kwa sasa wanapokelewa na kundi hatari la matumizi ya dawa za kulevya. Wapo hatarini mno. Leo au kesho, mitaa yetu itahathirika na hili tatizo. Mashirika ya kijamii, tokeni

Edit with WPS Office

mbele ya kamera zinazowamulika ili kuwatangaza katika runinga, nendeni mitaani mkawatoe. Juhudi zetu katika vita ya kupinga na kuzuia madawa ya kulevya basi iendane sawasawa na kuwatoa watoto wa mitaani katika vichochoro ambavyo ndio maeneo yanayotumika kwa biashara za madawa haya yasiyofaa katika jamii yetu. Ewe pwani ya Mombasa, safirisha hii barua kutoka katikati ya mji mkuu wa Tanzania, iwafike ndugu zangu wengine wengi katika nchi jirani. Waipokee na kuitilia maanani, Iwe sehemu ya mafundisho katika jamii zetu. Waibandike kile kona ya mitaa. Isomwe.

Madada poa, hili pia waliniambia nisiache kulisema. Mtoto wa kike wa mtaani habaki kuwa mtoto kila siku, miaka inakwenda, akitoka katika utoto anapokelewa na kundi la wadada poa, anauza mwili wake ili mkono uende kinywani. Msisahau, kumbukeni nilieleza kuwa wakiwa wadogo wengi wao wamekumbana na mateso ya kubakwa, wapo waliopata maambukizi ya virusi vya ukimwi, kati yao pia wapo madada poa. Ndugu zangu, mnafikiri afya za vijana wa kiume zitakuwa salama?. Vijana wa kiume ambao ndio wateja wa madada poa!. Wakina baba na kina mama, msipowasaidia watoto wa mitaani leo, kesho vijana wenu watakwenda kuwanunua kama madada poa kisha wataupata ukimwi. Wekeni jitihada leo. Tuwanusuru hawa watoto wasio na hatia. Tuwatoe katika jahazi la moto. Tuwasaidie wakawe watu wema.

Siwezi kusahau hili. Hili ambalo walitaka liwafikie wanaume kwa wanawake. Enyi wanawake kwa wanaume, starehe ya ngono inamatokeo mawili, mimba na maambukizi. Tujifanye tumesahau maambukizi. Vipi kuhusu mimba ?. Mimba ambazo baada ya miezi tisa mnajifungua na kutelekeza watoto. Mnahitaji elimu kiasi gani kufahamu kuwa mtoto utakayemtelekeza leo, ndio mtoto wa mtaani kesho?. Huenda dunia haitawahukumu lakini vipi kuhusu imani zetu, sote tunaamini yapo malipo siku ya mwisho. Tutalipwa ndugu zangu. Kumtelekeza mtoto ili awe mtoto wa mtaani sio jambo jema hata kidogo. Kama wewe usipoionea huruma damu yako unafikiri nani atabeba hiyo huruma?. Badilikeni. Mlee, akikushinda vipo vituo vya watoto yatima, kamkabidhi huko. Angalau utaepuka asilimia hamsini

Edit with WPS Office

za adhabu yako.

Halafu lipo ambalo walitaka niliseme. Walitaka niliandike kisha nilikemee. Vyombo vya usalama aya hii ni yenu, Hii barua pia naomba ifike katika meza zenu. Msome hii aya kwa umakini. Biashara ya binadamu inawahukumu sana watoto wa mtaani. Binadamu waliosahau neno “utu” wanawatazama watoto wa mitaani kama bidhaa za bure. Basi kama tumekubali kushindwa kuwalinda dhidi ya mbu wakali wanaowapatia malaria, basi tuwalinde dhidi ya hii hatari ya biashara ya binadamu. Watoto wa mitaani wanakutana ana kwa ana na mengi ya kutisha . Mengi mno. Vyombo vya usalama amkeni sasa, tazameni huku. Wapo binadamu wanaowategemea. Mtoto wa mtaani anahitaji ulinzi. Tuwalinde.

Mtoto wa mtaani pia anazo ndoto, ukosefu wa elimu umezika ndoto zao. Elimu ndio silaha muhimu ya kuwasaidia. Hata wao walikubali hili. Taasisi za elimu kuna dunia yenu inawahitaji kwa asilimia kubwa. Upo uhakika kuwa iwapo wakaipata elimu basi kuna asilimia nyingi za kuwabadilisha. Wakawa sehemu ya jamii ya kutegemewa katika mataifa yetu. Kutowapatia elimu ni kama tumeamua kusaini makubaliano ya wao kuwa watoto wenye tabia mbaya. Kisha na sisi tutajitoa ufahamu na kuwahukumu. Jirani Kenya, pokea barua hii, ukiisoma basi usisite kumpatia jirani mwingine, mpatie aisome. Kisha naye ampatie jirani yake. Afrika itambue kuwa watoto wa mtaani wanayo haki ya kupata elimu anagalau ya kusoma na kuhesabau.

Mwanangu kuwa, kuwa nikutume. Nikutume ukatazame. Nataka ukue ili uyaone. Mwanangu barua hii ukiisoma naomba ujifunze. Sio barua rahisi sana ila inamengi ya kukufundisha. Mwanangu mtoto wa mtaani ni nduguyo. Awe mweupe, awe mweusi. Ni ndugu yako. Mwanangu mtoto wa mtaani sio mbogo, sio chui. Ni mtoto anayehitaji upendo. Mwanangu ukikua utayaona mengi ambayo nimeandika katika hii barua. Mwanangu nawe usisite kuandika barua kama hii ikiwa utahitaji kunusuru kizazi kinachokulia mtaani. Mwanangu aya zinazofuata ni zako. Zisome nawe uzishike. Zikuelimishe. Ewe mwanangu umuonapo

Edit with WPS Office

mtoto wa mtaani usimkimbie iwapo hajakuonesha shari. Mtoto wa mtaani akikukwaza mwite chini kaeni zungumzeni. Liwapo tatizo basi limalizeni kwa upando. Ukihisi anahitaji kutenda baya mwonye kwa ulimi, mweleze madhara ya analotaka kulifanya. Kisha kama unacho msaidie.

Mwanangu usiwe mwepesi wa kunyanyua jiwe kumrushia mtoto wa mtaani pale ashikwapo kwa uwizi, hukumu nikazi ya sheria, usije ukahukumu mwanangu. Nataka ukumbuke kuwa malezi niliyokupa wewe, mtoto wa mtaani hajawahi kuyasikia popote pale sahau kabisa kuyapata. Mtoto wa mtaani anakosea kama binadamu wengine, kama wewe ukoseavyo. Msamaha pia ni sehemu ya haki yao kama mimi na wewe tukikosea tuombavyo. Mwanangu yashike hayo. Mwanangu ukiyapata maisha ya mia usisahu kutoa kumi zako kwa watoto wa mtaani. Wao hawajasoma ili waweze kuipata ajira ya milioni kama wewe. Kutoa ni moyo, mwanangu jitolee kwa watoto wa aina hii. Mwanangu kumchukua mtoto wa mtaani, kumsomesha na kumlea sio kosa. Fanya hivyo pale uonapo unaweza. Ni kweli huwezi kuwasaidia wote, ila mwanangu, kugusa ni bora kuliko kususa.

Mwanangu, ukikutana na viongozi wa madhehebu ya dini, waambie kuwa kuna salamu zao kutoka mtaani. Waambie kuwa mtoto wa mtaani anaomba zile shule wanazojenga ziwakumbuke na wao. Zisiwe shule za watoto wa wenye fedha na wanao jiweza tu. Wakumbushe kuwa dhamira ya dini ni kusaidia dunia, basi kama ni hivyo waeleze kuwa jamii inayowazunguka ndio dunia wanayotakiwa kuisaidia. Katika shule zao watenge madarasa kwa ajili ya watoto wa mtaani. Hili ni ombi tu, kumbuka kuwaomba. Mwanangu, nafahamu kuwa utaufikia ukubwa, nawe utatamani uwe na mtoto kama mimi. Sikukatazi, tafuta mwenzi wako. Ili mpate mtoto ila mwanangu kumbuka kuwa lazima mtoto utakayempata umlee wewe kama nifanyavyo mimi kwako. Nikukumbushe kuwa nyinyi ndio wazazi wa kesho. Wazazi ambao tunatamani msifanye dhambi ya kutelekeza mtoto. Hakika nathibitisha kuwa iwapo watoto wa sasa mkielewa vyema umuhimu wa kulea watoto wenu pasi na kuwatelekeza basi idadi ya watoto wa mtaani

Edit with WPS Office

itapungua.

Njia sahihi ya kumlinda mtoto wa mtaani ni kuipatia jamii yetu elimu tosha juu ya mtoto huyu. Wamtambue kama sehemu ya binadamua anayehitaji msaada zaidi kuliko kuhukumiwa kwa tabia mbaya. Ni lazima jamii zetu zielewe kuwa mtoto wa mtaani hakupenda kuwa vile alivyo. Tutake tusikate, jamii inatakiwa itambue kuwa inalo jukumu la kurejesha upendo kwa mtoto wa mtaani kwani sababu kubwa zinazotutenga nao ni jamii kuwatazama kama sehemu ya wanyama wakali wasiostahili kuwepo karibu nao. Hili ni tatizo. Upo umuhimu tena kwa uzito elimu juu ya mtoto wa mtaani ifahamike kwa kila mmoja wetu. Mashirika yanayohusika na afya hata elimu jamii, na haki za binadamu kwa ujumla yanatakiwa kulichukulia swala la mtoto wa mtaani kwa uzito wa tani za juu.

Vyombo vya habari amkeni. Acheni kueneza skendo na ushubwada katika magezeti yetu. Kumbukeni kuwa kuna mambo ya msingi ambayo mnayotakiwa kuyafikisha kwenye jamii zetu. Wamiliki wa runinga mpaka lini mtakazana kuonesha viumbe nusu uchi katika runinga!. Sikatai biashara ni muhimu mno katika runinga zetu ila baada ya hapo andaeni vipindi vya elimu juu ya jamii inayohitaji msaada wetu, watazamaji wenu watazame na kujifunza. Huu ni wakati sahihi wa kushirikia ili kunusuru maisha ya ndugu zetu waliosahaulika katika mitaa. Ewe Afrika yangu, wakumbushe viongozi wetu wanapokwenda kukopa fedha huko ughaibuni basi hizo fedha wakumbuke kuziwekeza katika kujenga vituo vya kuwalea watoto wa mtaani. Hatupingi ujenzi wa barabara ni wa muhimu mno. Ujenzi wa barabara ni sahihi sana, ila kama tukijenga na miundombinu ya kuwaweka salama binadamu wenzetu, basi hili litakuwa bora zaidi.

Ewe shirika la elimu kwa vitendo. Tazameni mitaani, toeni nafasi hata kwa uchache kuwapokea baadhi ya watoto wa mitaani. Mkiwapokea wafundisheni ujuzi kwa vitendo, ipo imani kuwa kama akijua kutengeneza iliyoharibika hawezi kuwa mwizi wa pale Dar es Salaam Chanika. Mtoto wa mtaani akipata ujuzi wa kujitafutia ridhiki bila

Edit with WPS Office

kukwapua cha mtu tutakuwa tumelisaidia taifa letu kwa ujumla.

Ndugu zangu nikimaliza barua hii bila kuandika yale yanayosemwa huku mtaani basi sitakuwa nimetenda haki, Yapo mengi yanasemwa. Haya yanaweza kuwa sehemu ya barua hii. Nitayanukuu bila kukwepesha lolote lile. Huku mtaani wanasema-nanukuu.“Tatizo ni wazazi kutokuwajibika. Kama watoto wamekushinda kulea kwanini uwatumie kuombaomba. Hii ni hatari sana. Wanaishi mazingira ya hatari kwa afya na usalama. Kumbukeni watoto wa mitaani hawatabaki kuwa watoto milele.Kama hawana wazazi ijulikane wepelekwe vituo vya kulea watoto yatima wapatiwe chakula, elimu na sehemu ya kuishi na watoto wenzao. Kama wazazi wako hai itabidi wazazi wachukuliwe hatua kali, maana wanawanyima haki watoto haki zao za msingi na kuepuka wajibu wao ambao ni kuwapatia mahitaji ya watoto wao, na si watoto kuwapatia mahitaji!. Itabidi watu wawe na leseni kuruhusiwa kuzaa. Kuzaa rahisi lakini kulea taabu. Hivi tutafika kweli? Vigogo hamuoni watoto mitaani , au mnatumia ndege kufika maofisini? Wanaosema si tatizo la serikali, ni kweli, ila wajibu ni wao kutilia mkazo juhudi za kuhakikisha kila mtoto anapata elimu haraka iwezekanavyo. Hawa watoto ni taifa la kesho.” ¬– “Jamii iwajibike. Jamii ya walikotoka na jamii wanamoishi. Hakuna mtoto aliyezaliwa mtaani, hivyo wanapaswa kurudi walipotoaka. Kuna watu wanaowatumia watoto kama chanzo cha kipato, hawa wachukuliwe hatua kali.”

omba omba hii ya watoto siyo tu ni aibu kwa nchi yetu bali na pia ni hasara kubwa kwa Taifa linalolilia maendeleo na kujitegemea. hawa watoto ambao ndilo Taifa letu la kesho-wanakua bila elimu ya msingi ya wazazi na pia bila elimu ya shule. Je ? watakuwa na faida gani kwenye Taifa la Mtanzania ? hawa watoto nao watakuja kuoa au kuolewa na kuzaa. Mimi naona , wakamatwe wapelekwe kwenye vituo vya watoto yatima ,huko watakula na watasoma na viwalo vya mitumba vipo watavaa na huko huko kwenye kambi za watoto yatima ,watatok madaktari na hata mawaziri.

Ujengeaji wa miji haswa inapokuwa jiji kubwa kama Dar es salaam

Edit with WPS Office

ndiyo chanzo cha matatizo yote(India ni mfano).Pia vituo vya watoto wa mtaani viwe mbali na miji ilikuwezesha watoto wawe karibu na mazingira hasili .Cha msingi ni kuongeza uwezekano wa maisha ya vijijini haswa unaozingatia maadili ya Taifa. Familia kujuwa haki ya mtoto kama mtoto, na mtoto kujuwa haki yake kama mtoto.Kuna familia zinasababisha watoto kutoroka nyumbani kutokakana na migogoro ama kumshirikisha mtoto kwenye utafutaji wa fedha ili familia ijikimu.Tuna mazingira mazuri na tukiyatumia basi watoto wanaweza kuridhika na kutokomeza hofu waliyo nayo ambayo mfano wake ndiyo huo wa kutafuta pesa ya muda na kujitenga na familia.

Sababu hawa watoto bado ni wadogo inabidi maamuzi magumu yafanyike, inabidi kama jamii tutengeneze nyumba zenye ulinzi mkali wa kuwaweka watoto huko (kuhakikisha kwamba hawatoroki) na huko wapewe elimu, wafundishwe tabia nzuri, na mbinu tofauti (tunapoteza vipaji vingi sana) na wakae huko mpaka pale wakiwa wakubwa (wahitimu ndio waachiwe waingie mitaani) na kama serikali iwape kipaumbele katika kazi tofauti. Na pesa na misaada yote iwe inapelekwa huko, na kuwa na ardhi ya kutosha kuwafundisha kilimo na ufugaji pia. Ninachomaanisha yaani hiki kiwe ni kama chuo cha kufundisha hawa ndugu zetu maadili mema ili tusaidiane nao kujenga taifa na sio kubomoa.-kwanza kabisa wajitokeze wanasheria au serikali iwe na wanasheria maalum wa kutetea watoto wanaodhulumiwa mali kama nyumba na ndugu wa wazazi pindi wazazi wanapofariki.

Kwa kweli hili ni tatizo kubwa sana hapa Tanzania maana ni kweli kila kona hawa wapo. Hawa watoto wengine wazazi wao walikufa kwa ukimwi na walezi/waangalizi waliobaki wanawanyanyasa ndo maana wanakimbilia mitaani na kuwa watoto kama hao. Jambo jingine kuna baadhi ya wazazi ambao wamezaa watoto wengi na kuwalea kukawa ni shida na hatimaye kutoroka nyumbani na kukimbilia mitaani. Wazazi tutafute njia mbadala kuwaokoa hawa watoto. Unakuta mwanaume mmoja anaoa wanawake wengi na matunzo kuwa shida. Nimewahi kushuhudia mkaazi mmoja katika kijiji kimoja huko Shirati Rorya aliyeoa wanawake 22 na hakuna hata mtoto mmoja aliyesoma na kuwa

Edit with WPS Office

na elimu nzuri. Sasa hali kama hii imepitwa na wakati.Tuelimishane ili tupunguze kasi ya hawa watoto.

Watoto wa mitaani wameongezeka, na wengi.wametokea mikoani kukimbilia kwenye majiji.Tatizo linaanzia kwenye familia, malezi kufikia mpaka binti kupata mimba, inakuja kijana aliyempa mimba na kuikataa.Hapo ndio familia inatakiwa isimamie malezi ya mtoto hata kama kijana kakataa, kinyume cha hapo, binti akifukuzwa ndio anamtupa mtoto.Wanawake km unaona huwezi kutunza mtoto tumia protection, matatizo yakikupata huyo kijana hutomuona.Mnatesa tu watoto mitaani.Nyingine ni wamama wa kambo nao wanachangia watoto kutoroka majumbani.Mwisho mimi nalia na Wizara ya Jinsia wanawake na watoto, hii wizara iko butu sn kushughulika na watoto wa mitaani. – Mwisho wa kunukuu.

Barua hii natamani naimaliza. Lakini bado natamani walau mtoto mmoja aisome mbele yenu, huenda ikwafikia wahusika katika sauti halisi. Sauti kutoka mtaani.

Edit with WPS Office